HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 07 Juni -Septemba, 2009

# Duncan Getakanod

## Mtoto wa Chifu aliyejitolea maisha na mali zake kutetea wafugaji wa Kibarbaig



Katika harakati za ukombozi popote duniani wamekuwepo watu ambao ni chanzo cha harakati husika. Watu hao wamekuwa wakisimama kidete kuhakikisha wanachokipigania kinafanikiwa. Mara nyingi watu wanaoongoza harakati hizo wamekuwa wakionekana wachochezi na kushutumiwa kuhatarisha amani kwa harakati zao hizo.

"Nimekuwa nikionekana mchochezi dhidi ya Serikali kwa kuwa nimekuwa nikiongoza wenzagu kuhakikisha Wabarbaig wanapata haki stahili ambazo kwa hakika tumekuwa hatutendewi."

Hivyo ndivyo anavyoanza kusimulia Mzee Duncan Getakanod ambaye ni miongoni mwa wanaharakati wanaotetea maslahi ya Wabarbaig hususani walionyang'anywa ardhi yao na kugawiwa lililokuwa Shirika la Chakula la Taifa (NAFCO) kuanzia miaka ya 70.

### NUKUU YA TOLEO

*Nenda mapumzikoni, umezaa wapambanaji wengi, ukibahatika kukutana na Mwl. Nyerere. Mwambie ile Ardhi aliyoinyakuwa kwa kigezo cha maslahi ya umma sasa imebinafsishwa iko mikononi mwa mabepari uchwara si NAFCO tena!*

Ng'wanza Kamata

Mzee Duncan ambaye kitaaluma ni Ofisa Mifugo taaluma ambayo aliipatia katika Chuo cha Mifugo Tengeru, Arusha mwaka 1961-1962, anasema kabla ya kuanza utetezi wa haki za Wabarbaig aliajiriwa kama Ofisa Kilimo katika tarafa ya Barbaig (sasa Wilaya ya Hanang').

Alifanya kazi hiyo kuanzia mwaka 1963-1966 na mwaka uliofuata aliajiriwa na benki ya CRDB mjini Arusha kazi aliyoifanya kwa mwaka mmoja 1967 - 1968. Baada ya hapo aliajiriwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kambi ya Oljoro.

"JKT kambi ya Oljoro Arusha niliajiriwa kama Ofisa Kilimo. Nilikuwa nikisimamia mashamba yote yaliyokuwa yakimilikiwa na Jeshi hilo nchini. Baada ya kufanya kazi kwa miaka sita kuanzia 1969-1974 nililazimika kustaafu kutokana na kuugua kila mara, lakini ugonjwa ulikuwa hauonekani. Nilihisi wafanyakazi wenzangu walikuwa wananiloga kwa wivu wa kupandishwa cheo kila mara,"anasema.

Baada ya kuacha kazi alirudi Katesh Hanang' na kuanza kazi ya utetezi wa haki za wananchi wa kabila la Wabarbaig ambao anasema walikuwa wakionewa kutokana na matukio mbalimbali ambayo yalikuwa yakitokea katika jamii hiyo.

Inaendelea uk. 3

## YALIYOMO

1 Tahariri Uk.2
2 Ujumbe wa HakiArdhi 4 na 5
3 Simulizi za waliomfahamu Dancan Uk. 6-11
4 Utenzi wa maombolezo - Shivji Uk. 12

**ARDHI NI UHAI ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mhariri**
Yefred E. Myenzi

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe

**Mchapishaji**
Alice Shamge

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.

Email:
**ecoprint@bol.co.tz**

# TAHARIRI

Kwa takribani miongo miwili sasa kumekuwa na vuguvugu la kijamii la kutaka mabadiliko katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Vuguvugu hilo, kwa sehemu fulani, ndilo lilitoa msukumo wa mageuzi ya mwaka 1992 nchi yetu ilipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa na kuruhusu asasi mbalimbali kufanya kazi za kijamii tukiwemo sisi. Wanaojihusisha na harakati hizi wamekuwa na majina mengi baadhi wakijipa wenyewe na mengine kuitwa na wanaowaona, kuwasikia au kushirikiana nao. Moja lililozoeleka sana kwa siku hizi ni wanaharakati. Karibu kila sekta au eneo la kijamii sasa ina wanaharakati.

Bila kwenda kwenye undani zaidi wa dhana hii, inaeleweka kuwa wanaharakati ni watu wanaoamini katika mabadiliko yenye taathira chanya kwa maisha ya mtu wa kawaida, na hivyo kutumia muda wao mwingi kuchochea, kuhamasisha, na kusababisha mabadiliko yenye mlengo wa kuleta usawa katika mahusiano hasa ya uzalishaji, umiliki na mgawanyo wa rasilimali baina ya makundi mbalimbali ya kijamii. Sifa yao kubwa watu hawa ni kujitoa, kujitolea na kujituma kupigania kile wanachokiamini kuwa kitaleta usawa katika mahusiano ya kijamii hata kama kwa kufanya hivyo itawagharimu maisha yao.

Ipo mifano lukuki ya watu wa aina hiyo lakini kwa leo tafakuri yetu inatuelekeza kumkumbuka ndugu Duncan Getakanod kutoka Wilaya ya Hanang Mkoani Manyara. Mzee huyu wa makamu ambaye sasa hatunaye tena, alikuwa jabali la harakati za ukombozi wa jamii ya Wabarbaig akijikita katika harakati za kutafuta haki ya milki ya ardhi kwa jamii hii tangu miaka ya 70 baada ya maeneo yaliyokuwa ya wafugaji kutwaliwa na serikali kwaajili ya kilimo cha ngano. Kwa kinywa chake, Duncan aliwahi kukiri kuwa yeye na jamii yake waliamini mambo yangeisha kwa muda mfupi kwa njia ya mazungumzo. Ndiyo maana akaongozana na wazee wenzake hadi viwanja vya Bunge na Ikulu, kwa makamishina na madarekta lakini kwa bahati mbaya sauti ya mnyonge haikupazwa vya kutosha kuwezesha milango ya wakubwa kufunguka. Ndipo ilipowalazimu kwenda mahakamani. Huko nako njia haikuwa nyoofu maana kesi zilizofunguliwa katikati ya miaka ya themanini, zimehitimishwa hivi karibuni na mahakama ya rufaa ya Tanzania mwaka 2006, kwa kutupilia mbali madai ya wananchi kwa vigezo vya udhaifu wa kisheria.

Anapofikia tamati ya maisha yake mwezi Juni 2008, Duncan analazimika kuamini kuwa kupaza sauti peke yake haitoshi, inabidi usikilizwe, na kuhamsisha peke yake hakutoshi, inabidi unaowahamasisha wahamasike. Anakata roho huku anasisitiza, ninyi wanaharakati ndio chachu ya mabadiliko, msikate tama, kuna siku haki itapatikana tu hata kwa Mbarbaig. Duncan anatuachia vitendawili kadha wa kadha vya kutegua juu ya mifumo yetu ya kiutawala. Je inamsikiliza nani! mnyonge au mwenye nguvu? Wawakilishi wetu wanasilikiza na kupeleka hoja za nani barazani? Je mahakama zinajali maslahi ya nani? Je mtu mnyonge aishiye kijijini anahaki gani katika mfumo wa utoaji na upatikanaji haki? Tusaidiane kutegua lakini Duncan alituasa kuwa tukiendeleza harakati ipo siku hoja zetu zitasikilizwa, na mabadiliko yatatokea.

Bila shaka ni wajibu wetu tuliobaki kujifunza kutoka kwa Duncan, moyo wa kujitoa, kujituma na kujitolea, pia ari ya kuhamasisha na kuchochea mabadiliko kwa jamii za wanyonge hata kama kwa sasa milango ni migumu kufunguka. Duncan pia ametuachia funzo kubwa la uvumilivu katika harakati. Kesi ziliduma kwa miaka zaidi ya ishirini lakini aliendelea kukatiza kwenye viambaza vya mahakama bila kukata tamaa. Yapo mengi yaliyosemwa dhidi yake yakiwemo ya kukatisha tamaa na kubeza jitihada za mapambano aliyoongoza. Lakini kwa moyo wake uliojaa ustahimilivu alibeba lawama zote dhidi yake bila kutetereka akichangamana na mahasimu wa kujitolea na wa kutumwa ili mradi alitambua alichokisimamia. Duncan hayuko nasi tena kimwili lakini kwa hisia nzito za ukombozi wa mtu mnyonge yuko nasi akituchagiza kuwa mwanaharakati kamili ni mtu mvumilivu, jasiri, shupavu na mwenye msimamo thabiti juu ya kile anachokipigania hata kama wote wanaomzunguka hawakiamini. Japo hatuko naye kimwili, lakini yu kati yetu kwa kazi alizofanya nasi. Buriani Duncan, baada ya kazi nzito uliyoifanya unastahili kupumzika kwa amani.

# Mtoto wa Chifu aliyejitolea maisha na mali zake

Inatoka Uk.1

Mzee Duncan anasema kuwa mwaka 1968 kwenye kijiji cha Wandelah katika tarafa ya Barbaig kulitokea mauaji ya raia mmoja mwenye asili ya Kiasia. Serikali iliwakamata kwa nguvu vijana wa Kibarbaig wakiwemo ndugu zake na kushitakiwa kwa mauaji ya raia huyo na kufungwa.

"Hapo ndipo naweza kusema nilipoanza rasmi utetezi wa haki za jamii ya Wabarbaig kwa kufuata wanasheria mbalimbali ili kuhakikisha watu waliokamatwa wanaachiwa na kurejea uraiani kwa kuwa walikuwa hawajafanya mauaji hayo zaidi ya kuonewa tu,"anasema.

Wakati akiendelea na utetezi huo huku wengi wa waliokamatwa wakiwa wameachiwa kutokana na utetezi waliofanya, mwaka 1976 kukatokea mauaji makubwa ya watu 23 katika kijiji cha Ihonda, Singida.

Akisimulia mauaji hayo Mzee Duncan anasema chanzo chake ni wizi wa ng'ombe ambao ulidaiwa kufanywa na vijana wa Kibarbaig ambao walikwenda katika vijiji ambavyo Wanyaturu wanaishi kuiba ng'ombe hao.


"Wanyaturu walifuatilia nyanyo za ng'ombe hao walioibiwa na kuishia katika moja ya nyumba ya Mbarbaig ambapo kwa kulipiza kisasi waliamua kuwachinja watoto watatu na wanawake wawili waliokuwepo nyumbani na wao kuondoka,"anasema.

Taarifa ilitolewa Polisi lakini hakukuwa na hatua zozote zilizochukuliwa, hivyo Wabarbaig wa eneo hilo wakaamua kuzika maiti hizo huku wakisubiri hatua za Serikali baada ya kutoa taarifa polisi. Matukio haya ambayo yalichochewa na wizi wa mifugo hasa ng'ombe yalizidisha uhasama kati ya Wabarbaig na makabila mengine na hivyo kuonekana kama ni jamii ya watu wakorofi wasiostahili kutimiziwa haki zao.

Duncan anasema mtizamo huo ndio ulikuwa kiini cha serikali kuwashitaki vijana wengi wa kibarabaig kila walipoonekana na hapo ndipo ukawa mwanzo wake wa kushirikiana na wenzake kuwatetea kupitia mifumo ya kiutawala na kimahakama pia.

Baada ya muda mrefu wa utetezi, mwaka 1978 kabla ya iliyokuwa tarafa ya Barbaig-kubadilishwa na kuwa Wilaya, Serikali iliwahamisha wananchi wa Kata ya Basout na kugawa zaidi ya ekari 30,000 za mashamba hayo kwa NAFCO.

Mzee Duncan anasema kuwa baada ya mgogoro



*Duncan Getakanod*

wa muda mrefu na Serikali dhidi ya mashamba hayo ikiwemo shamba la Mulbadaw ambapo wananchi waliokuwa katika mashamba hayo walilazimika kukimbilia katika Mikoa ya jirani, walilishitaki shirika hilo mahakamani.

"Mwaka 1984 tulishinda kesi dhidi ya NAFCO, wananchi wakaingia katika mashamba hayo kwa nguvu lakini walifukuzwa na Kikosi cha Askari wa kutuliza ghasia (FFU) waliotumwa na Serikali. Ndipo Serikali ilipokata rufaa kupinga hukumu hiyo lakini ilikuwa kwa siri kubwa ili tusijue,"anasema.

Mzee Duncan anasema ijapokuwa utetezi wa mashamba hayo umekuwa chanzo cha yeye kufilisika kwa kuwa amekuwa akiuza mali zake mbalimbali kwa ajili ya kuwasafirisha wananchi kwenda mahakamani kutoa utetezi dhidi ya mashamba ya NAFCO lakini bado hakukata tamaa.

"Tuliambiwa tuondoke katika mashamba hayo kwa kuwa sisi si wazalendo, tukakata rufaa nyingine kwa Rais lakini hakutusikiliza, Mwaka 1984 tukafungua kesi nyingine ya mashamba ya Gawal, Gidagamownd na Warret ambayo nayo tulinyang'anywa lakini hadi leo (2005) rufaa yetu haijasikilizwa baada ya kushindwa awali,"anasema.

Anasema katika safari ndefu ya utetezi hatasahau mwaka 1983 alipokamatwa na kuwekwa kizuizini kwa muda wa miezi isiyopungua sita kwa tuhuma za uchochezi, kadhalika mwaka 1984 na mwaka 1985 kabla ya kutolewa na kuitwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

"Baada ya kuwekwa rumande kila mara bila ya kufikishwa mahakamani, Rais Nyerere aliniita nikaenda Ikulu kuongea naye na ndipo tulipokubaliana kuanzishwa Wilaya ya Hanang' ili kuepusha baadhi ya migogoro iliyokuwepo. Ikaanzishwa kutoka Tarafa ya Barbaig.

Baada ya shuruba za utetezi wa muda mrefu, aliamua kujiunga na Chuo cha Siasa Kivukoni akisoma masomo ya Siasa ya Sayasi ya Jamii kama kada wa CCM na baada ya hapo aliendelea na utetezi wa ardhi iliyochukuliwa na serikali na kupewa shirika la NAFCO.

Anasema akiwa Kivukoni alikutana na Profesa Issa Shivji na kumweleza juu ya mgogoro huo wa ardhi wa mashamba ya NAFCO, na yeye kuanza kuufuatilia kwa karibu huku akiwapa msaada wa kisheria wa kuyakomboa mashamba hayo.

Mzee Duncan anasema wakati Profesa Shivji na wenzake kupitia Kituo cha Msaada wa Kisheria cha Chuo Kikuu Dar es Salaam wakiendelea na utetezi dhidi ya mashamba ya NAFCO mahakamani, lilianzishwa shirika la utetezi wa haki za ardhi la HakiArdhi na hapo likaanza kufuatilia mgogoro huo kwa karibu zaidi. Duncan akajiunga na shirika hili kwa lengo la kuongeza nguvu na chachu ya harakati za kutetea ardhi ya wafugaji wa Barbaig.

Mzee Duncan ni mtoto wa saba kuzaliwa kwa mama yake ambaye alikuwa mke wa saba wa Chifu Getakanod. Babu yake mzaa Baba yake Mzazi alikuwa Chifu aliyejulikana kwa jina la Gidamaosa Magena aliyeuawa na Wajerumani mwaka 1910. Babu yake mzaa Mama aliyeitwa Ninagi Gidasungo pia alikuwa Chifu wa Warbaig. Mzee Duncan alizaliwa mwaka 1935 Dongobesh. Alisoma shule hadi darasa la nne katika shule ya Msingi Dongobesh. Mwaka 1953 alijunga na shule ya kati hadi 1956 na mwaka 1961 alijiunga na chuo cha Mifugo Tengeru kusomea sayansi ya wanyama na kumaliza mwaka 1962.

Anatoa wito kwa wanasheria kutoa haki za watu bila upendeleo na kwamba sheria zifuate mkondo wake palipo na ukweli watoe ukweli. Alioa mwaka 1968 na amebahatika kuwa na watoto kumi akiwemo mmoja mwanasheria anayefanyia kazi zake jijini Dar es salaam.

Makala hii imenakiliwa kutoka katika gazeti la majira la Novemba 20, 2005. Mwandishi Seif Mangwangi alifanya mahojiano na Marehemu nyumbani kwake Katesh,Wilayani Hanang' Manyara.

# Ujumbe wa HAKIARDHI wakati wa mazishi ya Duncan

## PUMZIKA SALAMA NA KWA AMANI MZEE WETU DUNCAN GETAKANOD



*Ng'wanza Kamata - Mwenyekiti HakiArdhi akiwa na Duncan Getakanod*

Kila kinywa kitakuwa na lake la kusema, kila mwenye macho analo lake la kumtoa machozi, na kila mwenye moyo atakuwa na lake la kumuuma, na kila mwenye akili ana lake la kukumbuka, mwenye hisia ana lake la kumtia simanzi na kumsononesha. Hakuna kingine kinachoweza kuelezea hali hizi leo zaidi ya ukweli kuwa Mzee Duncan Getakanod aligusa nafsi na hisia zetu sote kwa namna mbalimbali. Duncan kaishi muda mrefu, kwa umri, hiyo pekee inatosha kumfanya awe na mengi aliyoyafanya katika maisha yake na kumkutanisha na watu wengi wa kila aina. Lakini kuna mengi zaidi katika maisha ya Duncan, na haya yanatokana na kazi zake alizozifanya katika maisha aliyoishi.

Kwetu sisi katika HAKIARDHI maisha ya Duncan tunayajua zaidi kwa upande wa harakati za utetezi wa haki za watu na hususan za ardhi. Lakini nyakati tulipopata fursa ya kumsikiliza Duncan akitusimulia hadithi za maisha yake ya kazi, tuligundua pia kuwa anayo hazina kubwa ya maarifa na ujuzi, uzoefu na mafunzo ambayo yametokana na misimamo aliyoichukua katika maisha yake toka akiwa kijana. Kutokana na simulizi zake chache tulizobahatika kuzisikia toka kinywani mwake ni vigumu sana, bila yeye mwenyewe kukusimulia, kuweza kuyaelezea maisha yake katika kina na mapana yanayostahili. Ndio maana mwenyewe akataka kutuachia kumbukumbu isiyofutika, ya kuyaandika yale aliyodhani yangekuwa ya manufaa na urithi kwa vijana wa sasa na wajao. Sisi katika HAKIARDHI tunajua alishaianza kazi hii, na baadhi yetu tulijitolea kusaidiana naye. Haitakuwa jambo baya kama kazi hii murua itaendelezwa na kukamilishwa hata wakati mwenyewe hawezi.

Maisha ya mwanaharakati kama Duncan ni ya kupigiwa mfano. Alijitolea kwa nafsi, hali na mali chache aliyonayo kuyaweka mbele maslahi ya wenzake na kuyapigania. Duncan hakuchoka pale wengine walipoanza kuchoka au kuchoka kabisa, hakukata tamaa pale wengine walipokata tamaa, hakutetereka pale wengine walipotetereka, hakurubunika pale wengine walipoanza kujichuuza na kutumia matatizo ya wengi wanaonyanyaswa na kugandamizwa kwa manufaa binafsi, na zaidi hakupoteza msimamo na mwelekeo hata pale vitisho vilipotumika na nguvu za dola zilipoelekezwa juu ya kichwa chake - wengi waliogopa na kuachia ngazi, lakini sio Duncan.

Wengine yawezekana wamekwisha sahau mapambano ya watu wa Wilaya hii ya HANANG na hasa kwenye maeneo ambako Serikali ilinyang'anya wenyeji mashamba yao na kuanzisha kilimo cha ngano chini ya NAFCO. Wanaokumbuka wanajua kilichotokea, msimamo wa wananchi na jinsi walivyopinga kudhulumiwa huko, na jinsi Serikali kwa kutumia mabavu ilivyowaondoa watu kwenye mashamba hayo. Hata baada ya kushindwa, wananchi hawakukata tamaa na waliweka matumaini yao kwenye vyombo vya kisheria - hususan Mahakama. Kesi za Halmashauri ya Kijiji cha Mulbadaw dhidi ya NAFCO ya mwaka 1985, kesi ya YOKE GWAKO na wenzake dhidi ya NAFCO ya 1988, na kesi ya AKO GEMBUL na wenzake dhidi ya NAFCO ya mwaka 1989 ambayo iliisha mwaka 2006, ni ushahidi tosha wa jinsi wananchi walivyojaribu kuitafuta haki yao kwa kila njia. Ni nani asiyejua kuwa uendeshaji wa kesi ulivyo wa gharama kubwa, na wenye adha na usumbufu mkubwa. Katika hali ya kawaida ni nani mwenye uvumilivu, nguvu, ari, ujasiri, nia na hamasa ya kuendelea kufuatilia kesi hizo hata baada ya kuchukua muda wa zaidi ya miaka 16. Katika watu wa aina hiyo, Mzee Duncan ni mmoja wao kama kesi ya kina AKO GEMBUL inavyodhihirisha. Wakati alioanza nao kesi walishaachia ngazi na ama kufariki, yeye aliendelea si tu kuzikumbuka bali pia kuzifuatilia.

Kwa tabia hii, wapo waliomwona Duncan kama mzee king'ang'anizi asiyeachia jambo mpaka alione mwisho wake, kama Mzee mkorofi kwa sababu tu hakuogopa wenye mamlaka ya kidola pamoja na vitisho vyao, japo yeye akiwaheshimu sana. Ama wengine walimwona kama mchochezi, kwa sababu tu hoja alizoziibua na mambo aliyoyaamini na kuyasimamia yaligusa maslahi ya wenye nacho na wenye mamlaka ya kiserikali. Lakini Duncan hakuwa na hila wala chuki na wale waliomwona jinsi walivyomwona. Lililomwongoza katika maisha yake, kwa jinsi tulivyomfahamu, ni chuki yake dhidi ya dhuluma, uonevu, unyanyasaji na ugandamizaji wa aina yoyote ile na unaofanywa na yeyote yule. Kupenda kwake haki na kuitetea kwake kwa wazi kulimjengea marafiki na maadui pia, lakini kwa ujumla wote kimemjengea heshima itakayoishi zaidi ya miaka aliyojaaliwa kuishi hapa duniani katika sura ya kiwiliwili ambacho leo tutakipumzisha hapa.

Inaendelea uk. 5

# PUMZIKA SALAMA - DUNCAN GETAKANOD

*Inatoka uk. 4*

Duncan alitambua kuwa katika kupigana dhidi ya dhuluma, uonevu, unyanyasaji na ugandamizaji, mtu mmoja peke yake hawezi. Ni kwa kulitambua hilo ndio maana Duncan alijishirikisha na watu wengine katika kujenga na kuimarisha nguvu na msimamo wa pamoja katika kuipigania na kuilinda haki. Ni katika imani yake hiyo Mzee Duncan alijiunga na HAKIARDHI na kuwa Mwanachama mwaka 1999. Hata kabla ya kujiunga na HAKIARDHI huko nyuma alikuwa amejishirikisha na wengine, hususan nyakati za mapambano ya wananchi wa Hanang dhidi ya Serikali iliyokuwa ikiwanyang'anya ardhi.

Duncan aliwaamini sana watu na hususan wasomi. Aliamini kuwa wao wanao mchango mkubwa sana katika kuzisaidia harakati za watu wanyonge kufanikiwa. Kwa imani yake hiyo alijishirikisha nao na kuwapa imani na matumaini yake na ya wenzake. Lakini mpaka anakufa, Duncan amebaini kuwa miongoni mwa wasomi wapo wasomi wa watu na wasomi dhidi ya watu. Harakati zake za kupigania na kutetea haki zimemfundisha kuwa wapo wasomi ambao kwa imani, mitazamo na misimamo yao wako pamoja na wameshikamana na wanyonge wale wanaotafuta ukombozi. Lakini alitambua kwamba wapo pia wasomi ambao ama hutumia shida za wanyonge kujinufaisha kwa kujifanya wameshikamana nao, au hujishirikisha na kushikamana na yale makundi ya watu na walio kwenye mamlaka kuhalalisha dhuluma, unyanyasaji, ugandamizaji, na udhalilishaji wa watu wanyonge. Kwa aina hiyo ya watu wanyonge ni taka taka ipaswayo kuondoshwa njiani na magugu yazuiayo mifumo ya kikandamizaji na kinyonyaji kushamiri - hivyo hawana budi kudunishwa zaidi na ikiwezekana kupatilizwa kabisa.

Pumzika Duncan wetu. Kazi uliyoifanya inatukuka. Mchango ulioutoa katika kujenga heshima ya binaadamu hatutausahau. Nenda mapumzikoni, wala usisite au kulalamika, kwa sababu yangalipo bado matumaini ya ukombozi wa wanyonge kupatikana. Umezaa wapambanaji wengi, nenda katusalimie waliokutangulia, mpe taarifa Chachage, Mekacha, na Kaare waambie yanayoendelea huku. Ukibahatika kukutana na Mwalimu Nyerere Mapema mwambie ile ardhi aliyoinyakua kwa kigezo cha maslahi ya umma sasa imebinafsishwa iko mikononi mwa Mabepari uchwara si NAFCO tena!

HAKIARDHI
6 JUNI 2008

# Mh. Diwani Rose Kamili:

## Duncan Kanifundisha upendo kwa watu na ujasiri wa kutetea jamii zinazokandamizwa; Ameacha pengo lisiloweza kuzibika milele

*Na Seif Mangwangi*

"...nilianza kumfahamu marehemu nikiwa mdogo, wakati akiwa mtumishi wa Serikali kama Ofisa mifugo katika Tarafa ya Barbaig sasa Wilaya ya Hanang'....nikamfahamu zaidi alipomuoa Dada yangu Mary mwaka 1968 na tokea wakati huo alikuwa mwanaharakati na mwenye upendo na wafugaji".

Hayo ni maneno ya mwanaharakati wa haki za binadamu na Diwani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Basout Wilayani Hanang' Manyara, Bi. Rose Kamili ambae ni shemeji yake na Hayati Mzee Duncan Getakanoda.

Anasema Marehemu akiwa Afisa Mifugo alikuwa akihudumia jamii ya wafugaji kwa kuwapatia dawa mbalimbali za kutibia mifugo yao kazi ambayo maranyingi alifanya bila ya gharama yoyote. "Wakati Serikali ilipochukua kwa nguvu mashamba ya Wabarbaig waliokuwa wakiyatumia kwa ajili ya kulishia mifugo yao kwa ajili ya shirika la Taifa la chakula (NAFCO), marehemu alikuwa wa kwanza kukemea tukio hilo na lilipokuwa kubwa zaidi aliamua kujitosa kupambana,"anasema.

Anasema Serikali ilichukua mashamba hayo ya Basout, Mulbadaw, shetchet, Gawal na Warret kwa nguvu huku ikiwaondoa kwa mabavu wananchi waliokuwa ndani ya mashamba hayo na kudhani hayakuwa na wenyewe na kwamba waliokuwa ndani yake walikuwa wavamizi.

"Serikali ilichukua mashamba ikidhani yapo tupu....ukweli maeneo yalikuwa na watu na nyumba zao zilikuwa ndani, kwa kuwa kwa desturi wafugaji hawana tabia ya kukata miti kabisa lakini watu walikuwa ndani ya mapori,"anasema Bi. Rose Kamili.

Anasema watu walitolewa kwa nguvu na operesheni hiyo ilianzia katika shamba la Mulbadaw na kueleza kuwa shamba hilo limechukuliwa kwa ajili ya kilimo cha ngano na mtu aliyekataa kuhama alizungukwa na mashine pamoja na matrekta ambayo yalikuwa yaking'oa miti iliyokuwa shambani na kuiangusha hovyo. " Matokeo yake watu walichomewa nyumba kwa sababu ilikuwa ni rahisi kufanya hivyo kwa kuwa ni maboma yaliyokuwa yamejengwa kwa nyasi zilizozungukwa na miti na hapo watu wakaanza kukimbia hovyo kwa kuwa hawakuwa na vitu vingi zaidi ya vyakula na mifugo yao,"anasema.

Akimuelezea Mzee Duncan, Bi. Rose anasema marehemu alikuwa akipigana kuhakikisha watu wanapata haki zao wasihamishwe kwenye mashamba hayo kwa kuwa walikuwa wakiyatumia kwa ajili ya kulishia mifugo yao. Anasema marehemu alikuwa anaelekeza watu namna ya kupata haki zao na mwaka 1981 akafanikisha kufungua kesi, kuhakikisha watu wanapewa ardhi yao baada ya kuondolewa kwa nguvu na kupelekwa kwenye maeneo ya mawe yasiyokuwa na rutuba.



*Mh. Diwani Rose Kamili:*

"Kesi ilikuwa inasimamiwa na wanasheria, kama kina Tenga na wenzake na yeye masaa yote alikuwa akifanya hiyo kazi kutembelea jamii na kuhakikisha anawaeleza kilichokuwa kikiendelea na hapo hapo akawa anauza hata mali zake *Inaendelea uk. 11*

# SIMULIZI ZA WALIOMFAHAMU DUNCAN GETAKANOD

## Mary Duncan:

### Mke wa Shujaa Hayati Duncan Getakanod aliyeunga mkono harakati za mumewe

*Na Seif Mangwangi*

"Ni mwaka mmoja sasa tangu Marehemu Mume wangu, Duncan Getakanod alipotutoka baada ya kuugua kwa muda mrefu. Si rahisi kusahau mambo mengi aliyoyafanya katika uhai wake ijapokuwa ni mengi alitarajia kuyafanya kabla ya kifo kumfika.

"Duncan alikuwa mtetezi wa haki za binadamu, Mwanaharakati aliyejitolea nguvu zake, mali zake na akili zake zote kuhakikisha anawatetea Wabarbaig kutokana na uonevu waliokuwa wakifanyiwa na Serikali iliyokuwa madarakani wakati huo".

Hivyo ndivyo Bi.Mary Duncan Mke wa hayati Duncan Getakanod anavyoanza kumzungumzia marehemu mume wake kama alivyomfahamu katika uhai wa maisha yake hadi kifo kilipomfika. Maria anasema Tanzania ingekuwa na watu watano aina ya marehemu Duncan wenye ujasiri wa hali ya juu na uzalendo na nchi yao haki za watu wanyonge zingeweza kupatikana na kuleta usawa kwa kila mtu.

"Nilianza kumjua Duncan Mwaka 1968 tulipokufunga pingu za maisha, nilifurahia sana maisha ya ndoa na mume wangu, alinipenda zaidi na mbali ya hilo alipenda sana ndugu na jamaa zetu hakuwahi nipiga zaidi ya kunieleza pale alipokwazika baada ya kumkosea,"anasema.

Ijapokuwa ni muda mrefu alikuwa akijitahidi kufanya utetezi dhidi ya manyanyaso ambayo wafugaji walikuwa wakifanyiwa, historia inaonyesha alianza rasmi kazi ya utetezi mwaka 1968 baada ya Serikali kuwakamata Wabarbaig wengi wakituhumiwa kumuua mmoja wa raia mwenye asili ya Kiasia na baadae mwaka 1976 Wabarbaig walipowaua Wanyaturu 23 na mwaka 1978 baada ya

Serikali kuchukua ardhi ya Wabarbaig na kuweka mashamba kwa ajili ya Shirika Taifa la chakula na Kilimo (NAFCO).

Aliwaunganisha Wabarbaig wachache waliokubali kuungana nae kwenda mahakamani kufungua kesi kuishitaki Serikali kutokana na hatua yake ya kuchukua ardhi ya Wabarbaig na kuigeuza mashamba ya shirika la Chakula la Taifa.



Mary Duncan

Marehemu alikasirishwa na vitendo ambavyo watendaji wa mashamba hayo walikuwa wakiwafanyia wafugaji ikiwemo kuteketeza kwa moto nyumba zao, kuchapa viboko Wabarbaig waliokuwa wakiishi jirani na mashamba hayo na kukamata hovyo mifugo ya jamii hiyo.

"Kweli hali hii ilimsikitisha sana Marehemu na kwa kuwa yeye binafsi alikuwa akipenda haki na usawa kwa kila mtu, alinieleza kuwa amesikitishwa na hali hii na hivyo anaamua kujitoa kuwatetea wafugaji hawa, mimi nikamkubalia,"anasema.

Anasema katika harakati hizo alionekana mchochezi na alikuwa akipigwa vita na watu wengi wa Chama na Serikali ikiwemo Wabarbaig waliokuwa wakinyanyaswa kwenye mashamba hayo kutokana na hofu kubwa waliyokua nayo baada ya kutishiwa vya kutosha na askari waliokuwa wakiwachomea nyumba zao.

"Walimu na wafanyakazi waliokuwa wakifanyakazi karibu na mashamba ya NAFCO na wenyewe walichukizwa na vitendo ambavyo wafugaji walikuwa wakifanyiwa, baadhi wakaungana na marehemu kuwatetea, wakajikuta wakisimamishwa kazi hata hivyo waliamua kujiondoa baada ya kusimamishwa kazi na kumuacha mume wangu akiendelea na harakati na hapo wakarudishwa makazini,"anasema.

Hata hivyo anasema Marehemu hakukata tamaa ya kuendelea kufanya utetezi dhidi ya mashamba hayo akiamini kwamba Mungu alikuwa pamoja na yeye katika kila kitendo alichokuwa akikifanya ili kuweza kunusuru maisha ya jamii yake.

Bi.Mary anasema anakumbua mwaka 1983 alipokuwa mzazi wa mtoto wa miezi miwili ambapo marehemu alikamatwa na kuwekwa kizuizini kwa zaidi ya miezi sita bila kushitakiwa akituhumiwa kufanya uchochezi dhidi ya Serikali.

"Niliteseka sana na wakati huo nilikuwa mzazi wa mtoto wa miezi mitatu anaitwa Daniel, ikanilazimu kuamka asubuhi saa 11 na kuwatayarishia watoto mahitaji muhimu hasa wanaoenda shule na baadae mimi mwenyewe niende shambani, maisha yalikuwa magumu sana,"anasema.

Anasema Mwaka 1985 Marehemu Duncan alikamatwa tena na kuwekwa kizuizini akituhumiwa kufanya uchochezi na wakati huo alikuwa mzazi wa mtoto mchanga aliyempatia jina la Dominick. Hapo ndipo alipopata msaada kutoka kwa mama yake mzazi aliyefika nyumbani kwake na kwenda Babati kujua hali ya mkwe wake.

"Alipoachiwa kwa mara nyingine nilimuuliza, kwanini anaendelea na hizo harakati wakati wenzake wengi wamekuwa wakimtenga na





kukata tamaa? Alinijibu kuwa, itakuwa haina maana kama yeye atanyamaza na kuendesha shughuli zake kusaka mali huku wenzake wakiteseka, hivyo akamtaka mkewe amwache awasaidie Wabarbaig kwa kuwa ni masikini, anasema na kuongeza:

"aliniomba nimuunge mkono kwenye harakati hizo nikakubaliana nae, kwa masharti kuwa yeye aendelee nazo na mimi niendelee na kazi yangu ya kufundisha kwa kuwa nilikuwa Mwalimu. Alikuwa akitumia mali zake kuhakikisha anakomboa ardhi ya Wabarbaig, aliuza mazao tuliyokuwa tunalima, alichukua hata na mshahara wangu wa ualimu kuwalipia nauli wafugaji wakati wa kufuatilia kesi zao"anasema.

Anasema mwaka mmoja (hakumbuki), marehemu akiwa na wenzake mkoani Arusha walipokwenda mahakama kuu kufuatilia kesi dhidi ya mashamba ya NAFCO waliishiwa nauli ya kurudi nyumbani ndipo alipoanza kutafuta msaada kwa marafiki zake na kuwasafirisha wenzake wawili wawili na mwisho alisafiri yeye.

Kuhusu Serikali kurudisha mashamba mawili ya Warret na Gawal kwa wakazi wa Hanang', Bi.Mary anasema Marehemu Duncan angekuwa hai angependa mashamba hayo yarudishwe kwa wafugaji ili waendeleze ufugaji.

Anasema shirika la NAFCO lilikufa kutokana na dhambi ya kunyanyasa watu iliyofanywa na viongozi wa shamba hilo na kuitaka Serikali kuomba msamaha kwa wafugaji kwa hasara iliyowapatia ikiwemo kuwanyanyasa na kuwarejeshea mashamba yao.

Akielezea maisha ya ndoa yake na Marehemu Bi.Mary anasema anakosa mambo mengi kutoka kwa marehemu ikiwemo upendo wake wa dhati aliokuwa akimuonyesha sanjari na kupenda ndugu jamaa na marafiki waliokuwa wakifika nyumbani kwao.

"Kila mtoto niliemzaa mimi, sikuletewa mtu wa kunisaidia, marehemu alikuwa akinipikia supu yeye mwenyewe alikuwa akiingia jikoni mbali ya kuwa na msaidizi wa kazi na wakati mwingine nilipokuwa sipo aliingia jikoni kupika, ilikuwa hakuna tofauti yoyote kama nilikuwa sipo,"anasema.

Anawashukuru wanasheria kama Profesa Issa Shivji, Profesa Luoga, Dkt.Mvungi, Profesa Mwaikusa, Dkt.Kapinga, HAKIARDHI kuweza kumsaidia marehemu kwenye harakati za utetezi wa mashamba ya NAFCO na kutoa wito kuendeleza harakati hizo ili haki iweze kupatikana.

## MZEE DUNCAN: Kweli Mapambano Hayana Mwisho!

Kama umewahi kusikia kuhusu migogoro ya ardhi huko Hanang, chanzo chake hakikutokana na wafugaji kuvamia mashamba ya wakulima. Kama huna tabia ya kutafuta taarifa, itakuwa ni rahisi kwako kuamini kwamba wafugaji wana ng'ombe wengi mno na wanahitaji kuwapunguza. Na pia unaweza kuamini hadithi za kwamba wafugaji wa maeneo hayo ni wasumbufu na wasiojali matakwa ya wanadamu wengine.

Hakuna mtu ambaye amewahi kufuatilia maswala yanayohusiana na migogoro ya ardhi huko Hanang' na asikutane na mtu ambaye wengi wetu tulimwita Mzee Duncan. Kwa wengi, Mzee Duncan anafahamika kama mkombozi wa wanyonge kwa watu wake, ambaye alikataa kuchukuliwa kwa ardhi na makazi yao. Mzee Duncan alikuwa mstari wa mbele katika kuongoza wazee wa eneo la Hanang waliokuwa wakikataa ardhi yao kuchukuliwa na kupewa wawekezaji na wao kuhamishwa.

Kukutana kwangu na Mzee Duncan wakati tukifanya tafiti mbalimbali na kushauriana na wana Hanang jinsi ambavyo wangeweza kutatua matatizo ambayo hawakuyaleta wao, kulinipa mwanga mwingine kuhusiana na migogoro ya ardhi kwenye Wilaya ya Hanang na Kilosa. Ila ambacho siwezi kusahau ni juhudi za Mzee Duncan katika kuwasaidia wana Hanang kupata ufumbuzi wa migogoro ya Ardhi.

Mara ya mwisho kukutana na Mzee Duncan ilikuwa ni miaka minne iliyopita kipindi hicho akiwa na miaka 'zaidi ya 85' wakati tulipokwenda kuendesha mafunzo yahusuyo haki na sheria za ardhi. Mzee Dancan alikuwa ndiye mwenyeji wetu, akituonyesha njia na kututambulisha kwa watu mbalimbali. Alikuwa akijumuika nasi wakati wa chakula na hata mara moja niliweza kumshawishi akanywa glasi ya divai!



*Agripina na Mzee Duncan*

Mzee Dancan alifahamika pale Hanang' kama mtu pekee ambaye hakukata tamaa ya kuendelea na kesi za kutaka kurudishiwa mashamba ya ngano waliyokuwa wamenyang'anywa hata baada ya kila mmoja wa wananchi wake kusahau.

Katika mazungumzo yetu, Mzee Duncan alinieleza kwamba hakuwa akipendwa na uongozi wa pale kwenye maeneo yake kwani alionekana kama ni mchochezi. Ni dhahiri kwamba viongozi hawakufurahishwa na juhudi zake za kutaka wananchi wa Hanang warudishiwe mashamba ya Ngano

Inaendelea uk. 8

# SIMULIZI ZA WALIOMFAHAMU

Inatoka uk. 7

waliyokuwa wamenyang'anywa zaidi ya miaka thelathini iliyokwisha pita na ambayo hayakuwa yakizalisha tena ngano kwa zaidi ya miaka 10! Alikuwa anasikitishwa na ukweli kwamba japo serikali ilikuwa imeyatelekeza mashamba hayo kwa muda wote huo, watu wa Hanang' hawakuwa na uhuru wa kuyatumia. Zaidi walipata vitisho vya kwamba endapo wataingia kutumia mashamba hayo wangeonekana wameingia kwenye mipaka isiyo yao.

Mzee Duncan hakuficha, ila alionyesha waziwazi kwamba wananchi wa Hanang walikuwa wamenyang'anywa ardhi yao. Pia alikuwa akionyesha wazi kwamba kunyang'anywa kwa mashamba ndicho kilichokuwa chanzo cha migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Zaidi aliamini kwamba chanzo cha umaskini waliokuwa nao watu wake ni kunyang'anywa mashamba yenye rutuba na kulazimishwa kuhamia milimani ambako ardhi haikuwa na rutuba na ilijawa na miamba na mawe.

Kama kuna watu ambao wanastahili kukumbukwa, Mzee Duncan atakumbukwa kama shujaa ambaye alipigania haki za wanyonge bila kuwa na chanzo cha mitaji ya kumsaidia ila tu kwa msukumo wa alichokiamini! Na kama kuna jambo ambalo ningependa wapenda haki walifuatilie ili kumleta Mzee Duncan karibu zaidi na watu aliowatetea ni kufuatilia taarifa za kitabu ambacho aliwahi kunieleza kwamba alikuwa ameandika. Nasikitika kwamba sikumshawishi anionyeshe kitabu hicho! Lakini ni matumaini yangu kwamba siku moja nitakutana na kitabu hicho kwenye Maktaba kwani tuna watu ambao wangependa kutafuta taarifa za kitabu hicho na hata kukifanyia kazi.

Kwa ufupi ni kwamba, Mzee Duncan ni mfano halisi wa wapiganaji wasiochoshwa na umri, kutokukubalika au hata kufilisika. Ni mmoja kati ya watu pekee waliopigania haki za wanyonge bila kujigamba na bila kutafuta kutambulika kwa juhudi walizozifanya!

# Prof. Luoga: Duncan aliamini kuwa Suluhu ya migogoro ya Ardhi ni kuheshimu haki sawa kwa wakulima na wafugaji

*"Ni Mtanzania aliyependa kupigania maendeleo ya jamii ya Wabarbaig akiamini rasilimali walizokuwa nazo ikiwemo Ng'ombe zitawasaidia kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini...aliwatembelea popote walipokuwepo hapa chini,".*

Haya si maneno ya mwingine bali ni Profesa Florens Luoga, Mkurugenzi wa masomo ya shahada Chuo kikuu Dar es salaam na mmoja wa wakurugenzi wa kampuni ya Wanasheria ya FK Chamber yenye makao yake makuu jijini Dar es salaam. Pengine utajiuliza ni nani anaetajwa na Profesa Luoga kuwa alipenda kuwapatia Wabarbaig maendeleo kutokana na rasilimali walizokuwa nazo, si mwingine zaidi ya Mwanaharakati Hayati Duncan Getakanoda.

Nilikutana na Mzee Duncan mwaka 1988 niliporudi nchini nikitokea Kanada nilipokuwa kimasomo na kukutana na kesi mbalimbali kuhusu mashamba ya NAFCO yaliyochukuliwa na Serikali na baada ya kusoma kesi hizo ambazo wanasheria wenzangu kina Shivji, Kapinga, Tenga na wengine wengi walipotumwa kama jopo la wanasheria wa (Msaada wa Sheria) Legal Aid kwenda Hanang' kufanyia utafiti madai ya wafugaji kunyanyaswa," anasema. Anasema safari ya wanasheria hao iliyokuwa ikiongozwa na Mzee Duncan kwa kuwapitisha katika maeneo mbalimbali na kuwahoji wahangawa zoezi la uhamisho, safari hiyo ilifanikiwa kwa asilimia mia moja"Mzee



*Prof. F. Luoga*

Duncan aliweza kufanikisha zoezi la kuwatembelea wahanga wa uhamisho kwa kuwa alikuwa akifahamu maeneo mengi sana ambayo yalivamiwa na watu waliteswa huku haki zao zikipokwa,"anasema. Anasema Mzee Duncan katika uhai wake alijaribu kuwaunganisha Wabarbaig kuwa kitu kimoja huku akipigania haki yao ya Kimsingi ya kupokonywa mashamba ya NAFCO na Serikali na kuanzisha mashamba ya Ngano kwa ajili ya akiba ya chakula cha Taifa na kwamba agenda yake kuu ilikuwa ni nini mustakabali wa maisha ya Wabarbaig hapo baadae na hapo alikuwa akijaribu kuwasiliana na maprofesa mbalimbali.

*"alikuwa na mawazo ya kuikomboa jamii ya wafugaji wa Kibarbaig, tulijikuta tukibishana kwa hoja mbalimbali na aliposhindwa aliondoka na kuwafuata maprofesa wengine kama shivji ama Dkt.Mvungi kujaribu kuwauzia hoja alizokuwa akifikiri na baadae alirudi kwangu kunieleza alichokubaliana kwa kushirikisha mawazo tofauti....hakika hakuna mwanaharakati mwingine nchini atakae kuwa jasiri kama* Duncan," anasema.

Prof. Luoga anasema katika uhai wake Mzee Duncan alifanikiwa kuwashawishi Wabarbaig wenzake kufungua kesi mahakamani wakipinga hatua ya Serikali kuchukua mashamba ya NAFCO huku wakisaidiwa na wanasheria wa chuo kikuu kutoka taasisi ya msaada wa kisheria (LegalAid).

Hata hivyo kesi mbalimbali za mashamba hayo zilionekana kushindwakufuatia kuingiliwa na wanasiasa mbalimbali ikiwemo viongozi ndani yajamii ya Wabarbaig waliokuwa na madaraka makubwa katika nchi pamoja nakesi hizo kukaa

Enaendelea Uk.9

## Duncan aliamini kuwa Suluhu ya migogoro ya Ardhi ni haki sawa

Inatoka Uk.8

mahakamani kwa miaka mingi bila kupatiwa hukumu.

"Mzee Duncan alikuwa akitetea wafugaji lakini Serikali ilikuwa ikitetea wakulima na kuonyesha ni kwa namna gani watanzania watawezakuondokana na umaskini kutokana na kilimo, Mawazo ambayo hayana tijakwa mfugaji aliyezoea kufuga...kwa hali hiyo Mzee Duncan alijikuta akipata upinzani mkubwa kutoka kwa baadhi ya viongozi wa serikalini ikiwemowaliokuwa wakitoka maeneo ya wafugaji.

Anasema mzee Duncan alifanya jitihada kubwa kuhakikisha nyaraka muhimu kuhusu kesi hizo zinapatikana ikiwemo mashahidi katika kesiwalizofungua kutoka mikoa ya Rukwa, Mbeya, Morogoro, Tanga n.k ambakowalikimbilia baada ya kuondolewa Hanang'.

Hata hivyo namkumbuka sana Mzee Duncan kwa harakati zake hasa kutoa elimu kwa wafugaji wa Kibarbaig kupitia tafiti mbalimbali ambazotulikuwa tukizifanya kama wanasheria ama mtu mmoja mmoja nakuhakikisha wanaelewa haki zao na kuondokana na woga waliokuwa nao.

Akielezea tatizo la wafugaji kuhamishwa kila mara Profesa.Luoga anasema maeneo mengi nchini yalikuwa yakimilikiwa na wafugaji lakini kutokana na ukosefu wa hatimiliki wakulima wamekuwa wakivamia maeneo hayo na kuanzisha kilimo baada ya kuyakuta yakiwa tupu.

"Meneo ya wafugaji mfano Wabarbaig yalikuwa yakienda hadi Dakawa mjini Morogoro lakini kwa kuwa hapo zamani hakukuwa na hati miliki wakulima walikuwa wakiingia kwenye maeneo hayo na kuanzisha kilimo na wafugaji walipokuta hali hiyo walijikuta wakihamia maeneo mengine, tatizo limeongezeka sana na ndio maana hivi sasa kuna migogoro mingi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji,"anasema.

Anasema wafugaji walikuwa wakihama kwenye maeneo hayo kupisha majani mapya yaweze kuota na baada ya miaka kadhaa hurudi tena katika eneohilo lakini ardhi hiyo ilionekana tupu na kuvamiwa na wakulima.

Profesa. Luoga anasema jamii ya Warbaig imepoteza mwanaharakati msomi aliyekuwa akitambua mipaka ya wafugaji hata maeneo muhimu ya kimila ikiwemo maeneo yenye miti ambamo wazee wa zamani wenye busara ndani ya jamii hiyo walizikwa ijulikanayo kama 'Bugheda'.

Kufuatia Serikali kurudisha mashamba mawili ya Gawal na Warret, Profesa Luoga anasema endapo Mzee `Duncan angekuwa hai angeshauri mashamba hayo yarudishwe kwa wananchi ili wapange matumizi yake wenyewe kwa kuwa Wabarbaig wamekuwa wakimiliki maeneo hayo kijamii(Communal) na sio kugawana kama ambavyo viongozi katika ngazi ya Wilaya wameelekeza ifanyike.

## MAYOMBA: Nilichukia Baba aliponikataza kusomea mazingira, akataka nisome sheria nitetee wanyonge

**"Hivi sasa nimeona umuhimu wake, natetea wanaoonewa kama yeye alivyofanya"**

*Na Mwandishi wetu*

Mayomba Duncan Getakanod ni mtoto wa Hayati Duncan Getakanod, mwanaharakati aliyefariki mwaka jana akiwa kwenye mapambano ya utetezi wa ardhi ya Wabarbaig iliyochukuliwa na Serikali na kuanzisha mashamba ya ngano chini ya shirika la Taifa la Chakula (NAFCO).

Akimzungumzia Baba yake, Mayomba ambaye ni Wakili anayefanya kazi katika kampuni ya uwakili ya FK Law Chambers na mmoja wa wamiliki wa kampuni hiyo anasema, marehemu Baba yake ameweza kuwarithisha tabia ya kupenda watu na kutetea binaadam wengine dhidi ya unyanyasaji wowote unaofanywa dhidi yao.

Anasema alianza kufahamu kuwa Baba yake ni Mwanaharakati wa haki za binaadamu mwaka 1979 alipokuwa akipambana na Serikali kuhakikisha inarudisha mashamba ya NAFCO kwa Wabarbaig baada ya kuipokonya kwa mabavu na kuanzisha mashamba ya ngano huku Wabarbaig wakijikuta wana tanga tanga huku na huko wakisaka ardhi ya kulishia mifugo yao.

"Binafsi nilianza kumfahamu Marehemu kwenye ulimwengu wa harakati mwaka 1979 nilipokuwa mdogo aliponiita na kunitambulisha kwa wageni wawili kuwa ni wajomba zangu na hivyo tangu wakati huo niwaheshimu kama ndugu zangu,"anasema Mayomba na kuongeza:

Alikuwepo mzee mmoja niliyetambulishwa kwa jina la Gidasayda Mang'ana na mzee mwingine aliyeitwa Francis Musey, ambao walikuja nyumbani kwetu Katesh na Baba aliniita akanitambulisha kuwa ni wajomba zangu ambao walikuja kutusalimu,"anasema.

Anasema kwa kuwa alikuwa hawafahamu watu hao, alimkubalia Baba yake lakini alibakiwa na swali ambalo alishindwa kulipatia jibu kwa kuwa siku zote alikuwa akiwafahamu wajomba zake isipokuwa hao wawili wapya aliotambulishwa siku hiyo.

Mayomba anasema baada ya miaka kadhaa kupita mwaka 1984 alikuja kugundua kuwa wale wazee aliotambulishwa walikuwa sio wajomba zake na kwamba Mzee Gidasayda Mang'ana alikuwa Mwenyekiti wa kijiji cha Mulbadaw na mwanaharakati wa utetezi wa shamba la Mulbadaw na mzee wa pili Francis Musey alikuwa wakili aliyekuwa akiwatetea dhidi ya shamba la Mulbadaw.

"Niligundua ukaribu aliokuwa nao Baba yangu na wazee wale ulitokana na harakati za kupigania haki ya Wabarbaig kurudishiwa shamba lao la Mulbadaw lililochukuliwa na Serikali na hapo ndipo nilikuja kugundua kumbe na Baba yangu alikuwa mwanaharakati wa haki za binadamu,"anasema.

Machi 1984 marehemu Mzee Duncan alimwamuru Mayomba kuchukua moja ya matrekta aliyokuwa nayo nyumbani kwake



Inaendelea Uk.10

# MAYOMBA: Nilichukia Baba aliponikataza kusomea.......

Inatoka Uk.9

pamoja na wenzake kwenda katika shamba la Mulbadaw kulima na kupanda ngano baada ya Serikali kuwapatia wananchi ushindi katika kesi iliyofunguliwa mahakama kuu.

"Tulikuwa tunalima huku watu wengine wakipiga kelele kuhamasisha wananchi walete mbegu tupande, walikuja kwa wingi tukapanda mbegu za ngano karibu shamba zima, wakati tunaendelea na kazi hiyo kikosi cha askari wa kutuliza ghasia (FFU) kutoka Babati kilikuja na kuanza kutusambaratisha kwa kutupiga mabomu ya machozi tuondoke shambani....kumbe baada ya kupata ushindi Serikali ilikata rufaa kwa siri na sisi hakutujua lolote,"anasema.

Anasema katika purukushani hizo anamkumbuka mtu mmoja aliyekuwa na asili ya kisomali Mohamed Abdivulet aliyejificha kwenye shimo la mchanga kukwepa kipigo cha FFU na mwingine alikamatwa akiwa anapanda mlima Hanang' ambapo katika kujitetea alidai kuwa alienda Katesh kusalimia ndugu zake na kwamba hakuwepo kwenye harakati za kulima shamba hilo.

Mayomba anasema mwaka 1985 akiwa anajiunga na kidato cha kwanza katika sekondari ya Ilboru mjini Arusha, alipata upinzani mkubwa kutoka kwa marehemu Baba yake ambapo wazee walifika nyumbani kwao kumfuata mzee Duncan waende Arusha kufuatilia kesi na yeye alikuwa akitaka fedha aende kujiunga na shule lakini marehemu Mzee Duncan alimnyima fedha ya kwenda shule na kumtaka abaki kwanza nyumbani mpaka arudi kwenye kesi.

"Nilikwazika sana wakati huo kwa kuwa nilichelewa kuanza shule kwa wiki kadhaa, na hapo nilikasirika na kuanza kuchukia harakati, cha kushangaza marehemu hakurudi nyuma, waliongeza tena kesi mbili kutoka kesi ya Mulbadaw zikafunguliwa kesi za Gawal iliyokuwa ikimhusisha Mzee Yoke Gwako na wenzake na kesi ya shamba la Warret iliyomuhusisha Ako Gambul na wenzake,"anasema.

Anasema Mama yake mzazi alikasirika na kuhoji kwa nini kesi hizo zimeongezeka kwa kuwa zilikuwa zinasababisha marehemu kutumia mali ya familia kuziendesha lakini Marehemu hakukata tamaa aliendelea kuzisimamia japo familia ilianza kuchukia harakati.

"Nikiwa nimemaliza kidato cha sita Sekondari ya Galanos nilipenda sana kuwa mwanamazingira kule chuo cha Mweka Kilimanjaro, lakini Prf.Shivji, Dkt.Mvungi, Dkt.Tenga, Prf.Luoga, Prf.Cris Mahina n.k wa kituo cha msaada wa sheria chuo kikuu, walimshauri Baba yangu nisomee sheria badala ya mazingira ili niwe mwanasheria, nikakataa na hapo ukatokea ugomvi mkubwa na Baba aliniambia ananipa elfu kumi na lolote likitokea nisimuulize kitu,"anasema.

Anasema alipokea hiyo fedha na kwenda Mweka kufanya mtihani wa kujiunga na chuo lakini aliporejea nyumbani aliamua kufuata ushauri wa Baba yake kwa kuwa alimuona kakasirika na kuamua kwenda chuo kikuu Dar es salaam.

"Nikiwa chuo kikuu nilikutana na kina Marehemu Chachage, Prf.Juma, Prf.Shivji, Dkt Asha Migiro, Dkt.Tenga wakanijenga vyema kisheria na hapo nikaanza kupenda harakati lakini hata hivyo nilipomaliza sikuweza kujihusisha sana na harakati kwa kuwa nilikuwa na majukumu mengine zaidi ijapokuwa Marehemu Babu alikuwa akinisisitiza kila mara kutetea wanyonge,"anasema.

Anasema wakati marehemu Duncan anasumbuliwa na maradhi baada ya kutoka Ihefu alipofuatilia sakata la wafugaji kuhamishwa na aliporudi kufikia nyumbani kwake jijini Dar es salaam, jopo la wazee watatu kutoka katika kijiji cha Vilima vitatu wakiongozwa na Mzee Giyam Marishi walifika nyumbani kwake jijini Dare es salaam na kumtaka kwenda vilima vitatu kuwatetea wafugaji waliopokonywa ardhi yao na mwekezaji kampuni ya EU UN Lodges.

"Baba alinisihi niwasaidie wale wazee na kwa kuwa nilikuwa napenda harakati niliwakubalia kuwatetea kazi ambayo tunaendelea nayo hivi sasa ili kuhakikisha lile eneo lao linarejeshwa katika himaya yao...niliingiwa na imani ya kuingia rasmi kwenye harakati baada ya Baba kunisihi kuwa jasiri, mkweli na mpambanaji hata kama kuna pingamizi niendelee tu kupambana hadi mwisho,"anasema.

Anasema familia yao ilifilisika sana kutokana na marehemu Duncan kutumia mali ya familia kuendesha harakati zake za ukombozi wa mashamba ambapo kutoka matrekta matano waliyokuwa nayo hivi sasa limebakia trekta moja tu.

Mayomba anasema kauli za wanasiasa zimekuwa zikikandamiza wananchi hasa wafugaji na kwamba kauli ya Waziri Mkuu aliyoitoa Bungeni katika kikao kilichopita baada ya Mbunge John Cheyo kuuliza hatma ya wafugaji wa Kilosa na kujibiwa kuwa 'kwani wametokea wapi' kwa maana warudi walipotoka, sio sahihi kwa kuwa wafugaji waliopo Ihefu na kwingineko nchini wengi wao walitokea Hanang' baada ya Serikali yake kuchukua maeneo ya wafugaji na kuyageuza mashamba.

# YOKE GWAKO: Hakuna kama Duncan tena, nitamkumbuka Daima


***Na Mwandishi wetu***

Mzee Yoke Gwako ni mmoja wa wazee maarufu katika Wilaya ya Hanang' na mmoja wa waliokuwa marafiki wakubwa wa marehemu mzee Duncan Getakanod kufuatia kushiriki pamoja kwenye harakati za mapambano ya ukombozi wa mashamba ya NAFCO.

Katika mahojiano yaliyofanywa nyumbani kwake katika kijiji cha Basout, Mzee Yoke Gwako mwenye umri wa zaidi ya miaka (80) anamtambulisha marehemu kama shujaa wa Wabarbaig atakaye kumbukwa daima katika maisha yake kutokana na harakati za mapambano dhidi ya mashamba ya NAFCO.

Anasema alianza kumfahamu marehemu miaka mingi iliyopita(hakumbuki), wakati huo akiwa mwanafunzi na baadae aliendelea kumfahamu kama Afisa Mifugo aliyekuwa akihudumia mifugo katika Tarafa ya Barbaig ( hivi sasa Wilaya ya Hanang').

Mzee Yoke Gwako anasema katika harakati hizo kwa kuwa Mzee Duncan alikuwa ni msomi aliweza kuwasaidia kuwapa elimu ya ujasiri wa kutetea haki zao pale ambapo walikuwa Inaendelea uk. 11



*Yoke Gwako.*

# Duncan Kanifundisha upendo

*Inatoka uk. 5*

ili kusaidia jamii ya Wabarbaig" anasema Bi. Rose Kamili ambaye pia ni Mke wa Katibu Mkuu wa CHADEMA Dkt.Wilbroad Slaa.

Anasema Hayati Duncan aliacha shughuli za familia na maendeleo ya nyumba yake kuhakikisha anasaidia wananchi kwa kulipia wenzake nauli kwenda Mahakama kuu mjini Arusha kufuatilia kesi ya mashamba ya NAFCO .

"Hata alipokuwa mgonjwa alikuwa anaendelea kutetea haki za hawa watu akitembea na ugonjwa wake bila kujali na mimi kama Diwani wa Kata ya Basout kwenye maeneo ya shamba la NAFCO aliweza kuja kwangu kunihimiza na kunitaka nifanye kazi bila kuogopa chochote nitetee haki za watu,"anasema. Anasema Marehemu alimtaka kutumia elimu aliyokuwa nayo kusaidia watu wengine na kumweleza kuwa watu wamekuwa wakiogopa Serikali kwa kuwa hawajasoma na hivyo kutojua haki zao.

Bi. Rose Kamili anasema watu wengi walikuwa wakiwekwa mahabusu baada ya kukamatwa kwenye mashamba ya NAFCO pale walipogoma kuondoka lakini unyanyasaji huo ulipozidi walihama katika maeneo hayo na kukimbilia maeneo mengine ya nchi ikiwemo Mbeya.

"Mwaka juzi alipokuwa anaumwa na wakati huo huo Ihefu kulikuwa na zoezi la kuwaondoa wafugaji, aliondoka na ugonjwa wake hadi huko akihamasisha wafugaji na wanasheria mbalimbali kuungana kuishinikiza Serikali kuwaacha wafugaji Ihefu, lakini hata hivyo kama tulivyosikia Serikali iliwahamisha kwa nguvu,"anasema.

Anasema pia marehemu atakumbukwa katika uhai wake kama mwanzilishi wa mashirika ya Kipok Barbaig na Burkarda yaliyoanzishwa kwa ajili ya kutetea wafugaji ili wapate haki zao za kimsingi na kuhakikisha wanaishi kwa amani kwa kushirikiana na shirika la Pingos Forum la Arusha.

Kuhusu kurudishwa kwa mashamba mawili ya Gawal na Warret, Bi.Rose Kamili anasema marehemu aliendelea na utetezi wa mashamba ya NAFCO ambapo mwaka 2002 alifanikisha kuzungumza na aliyekuwa Waziri Mkuu Frederick Sumaye kuhakikisha anarudisha mashamba hayo mikononi mwa wananchi. "Mwaka 2002 Serikali ilikuwa inabinafsisha mashamba ya NAFCO baada ya kufilisika na kushindwa kujiendesha, Marehemu Duncan akiwa na wazee wengine na baadhi ya madiwani, nikiwemo mimi tulienda kumuona aliyekuwa Waziri Mkuu Frederick Sumaye kuomba mashamba yarudishwe kwa wananchi badala ya kubinafsishwa,"anasema.

Bi. Rose Kamili anasema Serikali na jamii imepoteza mtu muhimu katika nchi kwa kuwa katika uhai wake marehemu alionyesha upendo kwa wote na ujasiri wa kutetea maslahi ya wanyonge hata pale walipopigwa mabomu kwa ajili ya utetezi na aliweza kusimamia kesi zote dhidi ya mashamba ya NAFCO mpaka mwisho wa uhai wake. Anasema athari ambazo Marehemu Duncan alizipata akiwa pamoja na wenzake akiwemo Mzee mmoja aitwae Jonas Gidasaida aliyepigwa na askari wa kutuliza ghasia (FFU) na kuvunjwa mkono, pia walichapwa viboko na kulazwa chini kwa kuwa walikuwa wanazuia mashamba hayo yasichukuliwe na Serikali.

Kwa upande wa familia Bi.Rose anasema Dada yake Bi. Mary Kamili (mjane), alikuwa anapata matatizo ya kuhudumia familia mwenyewe kufuatia shemeji yake (Marehemu Mzee Duncan), kuwa kwenye harakati.

"Hata hivyo leo hii tumegundua alikuwa anafanya kazi ya kusaidia watu katika utetezi, muda mrefu Dada alibaki na watoto lakini Mungu alimsaidia kufanya kazi zake vizuri ikiwemo kufundisha na ameweza kuwasaidia watoto wote kuwa wajasiri na wanaharakati wa haki za binadamu,"anasema.

Bi. Rose Kamili anamaliza kwa kusema, " Marehemu kabla ya kifo chake alinitaka nisiogope niendelee kutetea haki za binaadam na hata alipokuwa anaumwa na kushindwa kupumua aliniita, nikakaa nae pembeni na kuniuliza nini kilikuwa kinaendelea kuhusu mashamba haya mawili yaliyorudishwa ya Gawal na Warret, nikamjibu kuwa ugawaji wake bado sababu wananchi wanataka mashamba yagawanywe kwa wafugaji na sio kwa wote kwa kuwa mashamba yalikuwa ya wafugaji,".

# YOKE GWAKO: Nitamkumbuka Daima ...

*Inatoka uk. 10*

wakinyanyaswa na kuonewa na watendaji wa Serikali dhidi ya mali yao.

Anasema alikuwa akipita maeneo mbalimbali kuhamasisha wafugaji wakibarbaig kutoiogopa Serikali na badala yake wajitokeze kutetea ardhi yao ili warejeshewe na waweze kuendesha shughuli zao za kawaida.

Aidha mzee Yoke Gwako anasema nguvu iliyokuwa ikitumiwa na Serikali kupitia askari wa kutuliza ghasia (FFU), ziliwatisha wafugaji hao na kuamua kukimbilia katika maeneo mengine na wachache waliosalia walikimbilia kwenye maeneo ya mawe wakilisha mifugo yao kufuatia eneo lote lenye rutuba na majani kuchukuliwa na Serikali

"Marehemu alinisaidia sana kwenye utetezi wa mashamba ya NAFCO, alinisaidia kufungua kesi ya shamba la Gawal ambayo mimi ndiye niliyekuwa nikiongoza wenzangu na alihakikisha tunafika mahakamani kwa wakati…yeye alikuwa akitoa fedha ya nauli na sisi pia tulikuwa tukichangia nauli kama tulikuwa na fedha kama hatuna alikuwa anatoa yeye,"anasema Mzee Yoke.

Anasema walikuwa wakiuza mifugo waliyokuwa nayo ili kuweza kupata nauli na fedha nyingine kuitumia kwa ajili ya chakula na malazi pindi walienda mjini Arusha kufuatilia kesi yao na pale waliposhindwa kupatia soko mifugo yao waliweza kusafiri kwa ufadhili wa Duncan.


Mzee Yoke Gwako anasema Wabarbaig wamempoteza shujaa mpambanaji alieonyesha nia ya kuwasaidia kukomboa ardhi yao na kwamba haamini kama kutatokea mtu mwingine kama Marehemu Mzee Duncan kuweza kujitokeza kuwatetea Wabarbaig pasipo kudai gharama yoyote.

Akizungumzia mashamba mawili ya Gawal na Warret kurudishwa kwa wananchi,Mzee Yoke anasema hizo ni juhudi za marehemu Duncan na kwamba endapo leo hii angekuwa hai angependa mashamba hayo yarudishwe kwa wafugaji .

Anasema wafugaji ndio waliofukuzwa kwenye mashamba hayo na kuanzishwa mashamba ya Ngano kupitia shirika la NAFCO hivyo yarudishwe kwa wafugaji ili wapange namna ya kuyatumia kama ambavyo walikuwa wakifanya kabla ya kunyang'anywa kwa mabavu

HAKIARDHI ARDHI NI UHAI

# UTENZI WA PROFESA SHIVJI WA MAOMBOLEZO
## Buriani Mzee Duncan



Prof. Issa Shivji

### Kwa Nini?

*Mzee wangu, Mzee Duncan.*
*Mimi siyo mtunzi mashuhuri, wa shairi.*
*Mimi siyo mwandishi mahiri, wa riwaya.*
*Kwa kuomboleza kifo cha mzee wangu,*
*Sihitaji kuwa msanii.*

*Moyo wangu unadunda, unaimba.*
*Sauti inapepesuka,*
*Shairi inasuasua,*
*Riwaya inasononeka,*
*Wimbo unagomba.*

*Wasanii wamekuja juu,*
*Wote kwa sauti wananikaripia:*
*"Wee fedhuli wee,*
*Usitufedheheshe,*
*Usituaibishe.*
*Eti, unajifanya mtoto wa Mariam,*
*Kana kwamba unamiliki jina-Issa.*

*Potelea mbali,*
*Wasanii na usanii wao.*
*Leo nitaimba!*
*Nitajigamba, mimi Issa bin Mariam.*
*Nitaimba kuomboleza kifo cha Mzee wangu,*
*Mzee Duncan Getakanod.*

*Miongo mitatu iliyopita,*
*Tulionana, ukiwa kada wa chama,*
*Huko Kigamboni,*
*Chuo cha Kivukoni,*
*Kitovu cha itikadi,*
*Itikadi ya ujamaa.*

*Itikadi ukaisoma.*
*Ukaipapasa kwa undani,*
*Ukaipindua juu chini,*
*Ukaibua lukuki ya maswali,*
*Maswali yasiyo na majibu.*

*Kwa nini watu wangu, Wadatoga,*
*(Eti huitwa Wabarabaig!)*
*Kwa nini, hutekwa ardhi yao?*
*Kwa nini, hufa na mifugo yao?*
*Kwa nini, utu wao hudhalalishwa?*

*Mashamba yao hutaifishwa,*
*Mashamba yao hubinafsishwa.*
*Haki zao hupokonywa.*
*Kwa nini?*

*Kwa nini, binamu zangu Wamaasai,*
*Hukosa elimu, afya na maji?*
*Kwa nini wajomba zangu Wanyaturu,*
*Hubaguliwa, huadhibiwa kijumla?*
*Kwa nini?*

*Ukatembea na miguu,*
*Ukapanda mabasi,*
*Ukakodisha magari,*
*Ukaenda Dodoma.*
*Ukaonana na viongozi wa chama,*
*Heshima zao hazikukutetemesha.*
*"Kwa heshima na taadhima,*
*Nawaulizeni, siwadadisi, nawauliza tu:*
*Kwa nini watu wangu huteswa?"*

*Ukapanda mabasi, na treni,*
*Ukafika bandari ya salama.*
*Ukamwuliza Waziri Mkuu,*
*Ukuu wake haukukutisha.*
*Ukamuliza: Kwa nini?*

*Ukawalilia mawakili,*
*Mashauri ukayafungua,*
*Ushupavu ukauonyesha.*
*"Mashamba yetu ya ngano,*
*Mheshimiwa Jaji,*
*Yamefukiwa na buldoza,*
*Makazi yetu yamechomwa,*
*Jamii zetu zimesambaratishwa.*
*Je, hii ni haki?*
*Kwa nini?*

*Ushindi wa kimahakama,*
*Ukawa kilemba cha ukoka.*
*Ukakamatwa na polisi,*
*Ukawekwa ndani,*
*Ukafunguliwa mashtaka,*
*Eti, umediriki kudai haki za watu wako!*

*Mwanafunzi makini,*
*Mzee Ducan kajifunza,*
*Somo la awali:*
*"Naam. Wakubwa ni wakubwa!*
*Maslahi yao siyo yangu,*
*Maslahi yangu siyo yao."*

*Ukajiunga na HAKIARDHI,*
*Umoja ni nguvu, chombo ni muungano.*
*Mnyonge hana kabila,*
*Hana rika,*
*Hana jinsia,*
*Ana unyonge tu.*

*Hukuchoka, hukukata tamaa.*
*Vijana ukawashawishi,*
*Wazee ukawaunganisha.*
*Mapambano siyo lelemama,*
*Umoja wetu, ndiyo mkuki wetu.*
*Chombo chetu, ndiyo ngao yetu.*

*Buriani mzee wangu,*
*Mzee Duncan Getakanoda.*
*Kwa moyo mzito,*
*Anakuaga Issa bin Mariam.*
*Nenda salama, upumzike mahali pema.*

*Somo lako tutalifundisha,*
*Kamwe hatutalisahau.*
*Mapambano ni marefu,*
*Undani wake mjielewe,*
*Upana wake mjitambue.*

*Kamwe msisalimu amri,*
*Mbele ya ukatili, ukandamizaji na dhuluma.*
*Dhuluma ni adui,*
*Adui wa Wana wa Adamu.*

*Issa bin Mariam*
*Juni 03, 2008*

Anuani/Ofisi
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Kitalu Na. 236 Sinza Mori
S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu +255 22 2771360 /Faxi +255 22 2771362, +255 784 646 752.
Baruapepe: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org